BVOR

# Ofisi ya Blended Visa – Programu Rejelezi

## Makazi Mapya kwa Wakimbizi Kanada

## Taarifa Muhimu

Unataka kuja Kanada na maombi yako yameshafanyiwa mapitio ya awali na maafisa wa Kanada. Sasa unajiuliza/ungependa kujua nini kitafuata. Kuchaguliwa kwako kama mkimbizi unayestahiki ni hatua muhimu katika mchakato wa makazi. Lakini si hatua ya mwisho.

**Hizi ni taarifa kuhusu hatua zinazofuata katika mchakato, na kuhusu Kanada.**



Immigration, Refugees and Citizenship Canada
Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

Canada

© Kwa Heshima ya Malkia wa Haki wa Kanada, anayewakilishwa na Wizara ya Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia, 2019

Ci44-20/2019Sw-PDF
978-0-660-32881-2
2627-11-2019

# Ofisi ya Blended Visa – Programu Rejelezi

Unaweza kupatiwa makazi chini ya mpango wa Blended Visa. Hii inamaanisha kwamba serikali ya Kanada na kikundi cha udhamini binafsi watashirikiana katika kukusaidia kwa mwaka wako wa kwanza huko Canada.

Serikali ya Kanada itakupa msaada wa kifedha kwa miezi 6 utakapowasili Kanada. Serikali pia itagharamia huduma nyingi za afya/matibabu utakayohitaji utakapowasili.

Baada ya hapo, mfadhili wako atakupa msaada wa kifedha kwa miezi 6 mengine. Kwa ujumla, utakuwa na mwaka mmoja (1) wa msaada wa kifedha.

Mfadhili wako pia atakusaidia kihisia na kijamii wakati wa mwaka wako wa kwanza Kanada.

Unapounganishwa na mdhamini binafsi, unaunganishwa na kikundi cha watu wenye shauku ya kukusaidia kuzowea maisha nchini Kanada.

Watu hawa hawalipwi na serikali kukusaidia. Ni watu waliojitolea kukudhamini kwa sababu wanataka kusaidia. Makundi ya wadhamini hukusanya fedha na michango wao wenyewe kukusaidia.

Ikiwa unakuja Kanada kwa programu hii, utapata msaada kama wanaopata wale ambao wanasaidiwa na Mpango wa Wakimbizi wa Serikali. Zaidi ya hayo,

utapokea msaada wa mdhamini binafsi kukusaidia kuzowea maisha nchini Canada.

Unahimizwa kuwasiliana na wadhamini wako wakati unasubiri kuthibitishwa kuja Kanada. Hili linaweza kufanyika kwa barua pepe, kupiga simu au kutuma ujumbe mtandaoni.

## Mchakato wa maombi - hatua zinazofuata:

- Wewe na familia yako ni lazima mpimwe afya kabla ya kuja Kanada.
- Gharama za kufanya vipimo vya afya, pamoja na huduma nyengine za afya kabla ya kuondoka, zinalipiwa na serikali ya Kanada.
- Inaweza kuchukua miezi kadhaa baada ya usaili wako kabla ya kutakiwa kwenda kufanya uchunguzi wa afya. Shirika la Kimataifa la Uhamiajii (IOM) au Ofisi ya Uhamiaji, Wakimbizi naUraia Kanada (IRCC) watawasiliana na wewe kwa taarifa zaidi kama ukiwa bado hujafanya vipimo vyako.
- Ni lazima pia ufanyiwe uchunguzi wa historia ya masuala ya uhalifu na usalama. Hii ni kuhakikisha kuwa hujawahi kufanya uhalifu mkubwa, na pia wewe si hatari kwa usalama wa Kanada.
- Maafisa wa Kanada wataangalia maombi yako na kuamua kama umefaulu uchunguzi wa afya, usalama na uhalifu. Isipokuwa kama utatakiwa kufanya hivyo, hakuna haja ya kuwasilisha maelezo yoyote ya ziada.
- Kama hutofaulu uchunguzi wako wa afya na wa mambo ya usalama na uhalifu, unaweza usichaguliwe kuja Kanada.
- Kama utafaulu uchunguzi wako wa afya, na mambo ya usalama na uhalifu, Kanada watawaomba Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), au shirika jengine, kukusaidia kujiandaa kuja Kanada.

- Katika baadhi ya nchi, utaalikwa kuhudhuria madarasa ya bure ya maelekezo kabla ya kuondoka. Madarasa haya ya bure, yanaitwa Maelekezo ya Kanada kwa Nchi za Nje, yanalipiwa na serikali ya Kanada na hutolewa na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM). Katika mafunzo haya, utajifunza kuhusu Kanada na huduma zinazopatikana za kukusaidia baada ya kufika kwako.
- Kama hujaalikwa kuhudhuria Mafunzo ya Nje ya kuhusu Kanada kwenye nchi yako, wajulishe wadhamini wako na watahakikisha unayapata utakapofika Kanada.

## Kuondoka kuja Kanada:

- Mara baada ya kufaulu uchunguzi wote na hati zako ziko tayari, safari yako ya Kanada itaandaliwa.
- Katika baadhi ya nchi utahitajika kulipa ada ya kuondoka kwenye serikali ya nchi ambayo ulikuwa unakaa kabla ya kuondoka. Wakati unahitajika kulipia ada hii peke yako, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) linaweza kukusaidia katika mchakato huu.
- Kama huna pasipoti au hati nyingine halali za kusafiria, serikali ya Kanada itakupa hati ili uweze kusafiri kuja Kanada.
- Serikali ya Kanada itatoa mkopo kufidia gharama za kusafiri kwako kuja Kanada.
- Fedha hii ni mkopo, ambayo ina maana kwamba utatakiwa kuilipa serikali kiwango chote ndani ya miaka mitatu (3) hadi minane (8), kulingana na kiwango cha mkopo.
- Ni lazima uanze kulipa mkopo ndani ya mwaka mmoja (1) baada ya kufika Kanada. Mdhamini wako hatolipa mkopo wako.
- Utapewa msaada wa kwenda uwanja wa ndege na kushughulika na maafisa wa uhamiaji wakati unapoondoka.
- Kusafiri kwenda Kanada mpaka kufika kwenye kituo chako cha mwisho inaweza iwe ni safari ndefu sana. Unaweza kuchukua vitafunio vyako kwa sababu unaweza ukapaswa kulipia chakula chako kwenye ndege au uwanja wa ndege.

## Kufika Kanada:




- Utakapofika Kanada kwa mara ya kwanza, wafanyakazi kutoka shirika la kutoa huduma, ikiwa ni pamoja na mkalimani kama anahitajika, watakupokea utakaposhuka kwenye ndege na kukusaidia katika taratibu za uhamiaji.
- Ikiwa unaunganisha ndege, watakuongoza mpaka mwisho wa safari yako. Pia watakupatia chakula na mahali pa kulala kama unapaswa kusubiri kwa masaa mengi kabla ya kupanda ndege nyengine.
- Kama tayari umefika katika kituo chako cha mwisho, watakukutanisha na mdhamini wako ambaye atakuwa anakusubiri uwanja wa ndege.
- Mdhamini wako atakupatia sehemu ya kukaa, kama apatiment, nyumba au hoteli.
- Wakati mwingine unaweza kupewa makazi ya kukaa kwa muda mfupi wa siku chache au wiki kadhaa mpaka utakapohamia kwenye makazi yako ya kudumu.
- Mdhamini wako anaweza kukupatia baadhi ya vitu mara ufikapo na watakusaidia kununua chakula na mavazi yako mwenyewe kwa msaada wa kifedha wanaotoa.
- Unaweza pia kupatiwa nguo za baridi.
- Mdhamini wako atajibu pia maswali yako yote kuhusu maisha ya Kanada na kukusaidia:
    - o Kutafuta wakalimani;
    - o kutafuta daktari wa familia na daktari wa meno;
    - o kuomba bima ya mkoa ya huduma za afya;
    - o kuandaa watoto wako kwenda shule;
    - o kukutana na watu mnaolingana kwenye vitu mnavyopenda;
    - o kutumia huduma za benki, usafiri n.k na
    - o kukuunganisha na huduma za maandalizi zinazodhaminiwa na serikali kama vile mafunzo ya lugha, huduma za ajira, na nyenginezo.

Serikali ya Kanada na Mdhamini wako watakupatia msaada wa awali kukusaidia kuanza maisha yako nchini Kanada. Lakini ni muhimu kwako kuwa na matarajio ya kiuhalisia.

Lazima uwe tayari kufanya kazi kwa bidii ili kufanikiwa sana katika maisha yako nchini Kanada.

Msaada wa kifedha kutoka serikalini na kutoka kwa mfadhili wako binafsi ni wa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe unayofika, au mpaka utakapoweza kujitegemea - chochote kitakachokuja kwanza. Unapaswa uweze kujikimu mwenyewe na familia yako baada ya mwaka mmoja.

# Makazi na familia yako



Wewe na mwenza wako, watoto wako wanaokutegemea, na watoto wako wanaokutegemea wenye watoto wanaowategemea, wanaweza kuomba pamoja kwenye fomu moja unayoomba ya uhamiaji  na kuja Kanada pamoja.

Ikiwa kuna **mabadiliko yoyote** kwenye hali ya ndoa (kwa mfano, umeoa/umeolewa au umeachwa/umeachwa kwa talaka), au kama utapata mtoto wakati wowote kabla ya kusafiri kuja Kanada, **lazima** uwataarifu maafisa wa UNHCR pamoja na maafisa wa Kanada. Ili wanafamilia wako wapya waweze kuingizwa kwenye maombi yako ya uhamiaji.



Ni **muhimu** sana kumwambia mdhamini  wako na maafisa wa Kanada kwamba mnataka kuishi kama familia. Ni lazima  uorodheshe wanafamilia wako  wote kwenye maombi yako. Kama hutowataarifu  maafisa wa Kanada kuhusu mke/mume wako au mtoto wako kabla ya kuondoka kuja Kanada, hutoweza kuwadhamini kuja Kanada hapo baadae.

Kama una ndugu au rafiki wa karibu waliopo Kanada tayari, na kama ungependa kuishi karibu nao, unapaswa kuwajulisha sasa hivi maafisa wa UNHCR na  maafisa wa Kanada. Kadri iwezekanavyo, Kanada wanajaribu kuwapatia makazi wakimbizi ambapo wanaweza kupata msaada kwa watu wanaowafahamu.

Kwa sababu utapewa makazi mapya kupitia BVOR Blended Visa – Programu Rejelezi,  utapangiwa mji, jiji moja au eneo la jirani lililopo karibu na kikundi cha wafadhili  wako walipo. Ikiwa una jamaa au unafahamiana na watu kwenye jamii ambapo mdhamini wako anakaa au ana mwakilishi, watajaribu kukuweka kwenye jamii hiyo.

Kama ndugu zako au watu wako watahamia kwenye mji mwingine Kanada, tafadhali  mtaarifu mdhamini wako mapema iwezekanavyo ili  muweze  kushirikiana katika kuangalia kama kuna msaada wa kutosha wa makazi kwenye jamii mpya.

Unaweza ukawa umewaweka kwenye maombi yako wanafamilia wanaokutegemea ambao huendi nao Kanada.  Mara ukishatulia Kanada, unaweza ukawaleta Kanada wanafamilia wako hawa kwa kupitia mpango unaoitwa Fursa ya Dirisha la Mwaka Mmoja (OYW). Unaweza kuomba ndani ya mwaka mmoja baada ya kufika kwako Kanada, kumleta mwenza wako anayetambulika kisheria, mtoto anayekutegemea, au mtoto anayemtegemea mtoto wako anayekutegemea kukaa na wewe Kanada, kama tu waliorodheshwa kwenye maombi yako kabla hujaondoka kuja Kanada.

Wanafamilia wengine, kama wazazi, babu na bibi, au kaka na dada, watapaswa kutuma maombi yao peke yao ili wazingatiwe kwenye kupatiwa makazi. Mara ufikapo Kanada, unaweza kudhamini wanafamilia kuhamia Kanada kama utakidhi  vigezo kadhaa. Vyovyote vile, hatua za kuleta wanafamilia hawa Kanada inaweza kuchukua muda mrefu, na unaweza usiione familia yako kwa miaka kadhaa.

IRCC  haitochangia kusafirisha wanyama labda kama kuna mnyama anaetoa huduma ambapo kuna sababu muhimu iliyopo ya kuwasafirisha kuja Kanada. Wakimbizi lazima wafanye wenyewe utaratibu wa kusafirisha wanyama wa nyumbani.

## Hali yako ya uhamiaji

Unapofika Kanada, utapewa hati inayoitwa Uthibitisho wa Makazi ya Kudumu (Confirmation of Permanent Residence – COPR) inayosema unaweza kuishi hapa kama **mkazi wa kudumu**. Hii inamaanisha kwamba kisheria unaweza kukaa Kanada maisha yako yote. Utaweza kufanya kazi au kwenda shule.

Kuna masharti maalumu ya muda gani unapaswa kuishi, na kuwa, Kanada kabla ya kuomba uraia wa Kanada. Utakapokidhi vigezo vyote, unaweza kuomba kuwa raia wa Kanada.

Taarifa zaidi zinapatikana kwenye [https://www.canada.ca/en/immigration-refugees-citizenship/services/canadian-citizenship/become-canadian-citizen.html](https://www.canada.ca/en/immigration-refugees-citizenship/services/canadian-citizenship/become-canadian-citizen.html) au kupitia kikundi cha wadhamini wako.

## Utaishi wapi Kanada

Kanada ni nchi ya pili kwa ukubwa duniani, yenye miji mingi lakini pia yenye maeneo mengi ambayo kuna watu wachache au hakuna watu wanaoishi. Miji mingi mikubwa iko sehemu ya kusini mwa Kanada, karibu na mpaka wa Marekani.





Maeneo mengi ambako watu wanaishi yapo mbali mbali na huchukua muda mrefu kufika huko, hata ukisafiri kwa ndege. Kwa mfano, umbali kati ya miji mikubwa ya Kanada, Toronto na Vancouver, ni zaidi ya kilomita 4,300, au karibu siku 3 kwenda na basi.

Utapangiwa kwenye mji au jiji ambalo kundi la wadhamini wako wapo.

Wadhamini wamejitolea kukusaidia kwa kuelewa kuwa utaishi kwenye jamii yao na kufanya nao kazi ili uweze kujitegemea. Japokuwa una haki ya kuhamia popote pale Kanada, wadhamini wanatakiwa kukusaidia kwa mwaka wako wa kwanza tu **wakati upo kwenye jamii yao**.

Kama utaamua kuhamia sehemu nyingine ya Kanada, wadhamini wako wanaweza wasiweze kukusaidia kifedha na unaweza ushindwe kupata misaada ya huduma za serikali.

## Jamii ya Kanada



Nchini Kanada, wanaume na wanawake ni sawa. Wana haki sawa na wanahudumiwa kwa kiwango sawa cha heshima. Wanaume na wanawake wa  tabaka zote za kijamii, tamaduni, kabila na dini wanashirikiana na hutendewa sawa.

Upo huru kuzungumza maoni yako nchini Kanada, wakati ukiheshimu haki ya wengine kufanya hivyo.

Kuna makundi mengi ya jamii na vyama vya wanaume, wanawake na watoto ambavyo unaweza kujiunga. Unaweza kushiriki katika shughuli za michezo kama vile soka au kuogelea, na kuna shughuli nyingi ambazo unaweza kufanya kama familia. Baadhi ni bure, wakati shughuli  nyengine zina malipo.

Unaweza kuwa umezoea kuwa pamoja na familia yako kukuunga mkono na  kukusaidia. Ukiwa Kanada, unaweza kujisikia mpweke, lakini huko peke yako. Kama una wasiwasi, wasiliana na wadhamini wako au uongee na mtu kwenye jamii yako. Kuna watu hapa ambao wanaweza kukusaidia kukabiliana na maisha nchini Kanada.

Kama kuna mikutano ya wageni katika eneo lako, jaribu kuhudhuria. Hii itasaidia kupata  marafiki kwenye jamii na kukusaidia kufahamu huduma katika eneo lako.

## Sheria za Kanada




CSheria za Kanada hutambua na kulinda haki za msingi na uhuru  wa kila mtu, ikiwa ni pamoja na uhuru na usawa. Mkataba wa Kanada wa Haki na Uhuru ni sehemu ya Katiba ya Kanada. Inakulinda mara tu ufikapo Kanada.

Tambua kuwa kuna baadhi ya vitendo ni kinyume cha sheria nchini Kanada ambavyo vinaweza kuwa si kinyume na sheria nchini kwako unapoishi. Ni kinyume cha sheria na ni kosa la jinai kupiga mwanamke au mtoto, kuacha watoto bila ya uangalizi wa mtu mzima, kuendesha gari bila ya bima au leseni, au kwa watoto wadogo kusafiri kwenye gari bila ya kiti cha gari. Pia ni kinyume cha sheria  kujisaidia hadharani haja ndogo au haja kubwa, hata hivyo kuna vyoo vingi vya bure katika maeneo mengi.

Kwa taarifa zaidi za sheria za Kanada na mfumo wa haki zinapatikana kwenye tovuti ya serikali ya Kanada ukurasa wa tovuti.

## Lugha




Kanada kuna lugha 2 rasmi: Kiingereza na Kifaransa. Ni muhimu kufahamu Kiingereza au Kifaransa ili kukusaidia kuishi Kanada.

Kiingereza ni lugha inayozungumzwa zaidi katika mikoa na wilaya nyingi. Kifaransa ni lugha kuu inayozungumzwa Quebec, ingawa kuna jamii za Kifaransa katika mikoa yote na maeneo yote nchini Kanada. Pia kuna wakazi wachache ambao wanazungumza Kiingereza Quebec.


Kiingereza au Kifaransa kizuri kitakusaidia kupata kazi, kwenda shule, kupata huduma na kupata marafiki. Kama inawezekana, jaribu kuboresha Kifaransa au Kiingereza kabla ya kuja Kanada.

Mara ufikapo Kanada, unaweza kujiunga na madarasa ya bure ya lugha yanayofadhiliwa na serikali bila ya gharama yoyote. Wadhamini wako watakusaidia kukupa taarifa ya namna ya kutathminiwa viwango vyako vya lugha na namna ya kujiandikisha kwenye programu za mafunzo ya lugha.

## Kutafuta kazi







Ingawa wewe na familia yako mtapata msaada wa kifedha kwa mwaka wako wa kwanza nchini Kanada, ni vizuri kujiandaa kutafuta kazi ili uweze kujikimu wewe na familia yako.

Kadri unavyozungumza Kiingereza au Kifaransa vizuri, itakuwa rahisi zaidi kupata kazi. Kazi nyingi zilizopo na biashara zinahitaji:

- kuzungumza Kiingereza au Kifaransa vizuri,
- kuwa na ujuzi mkubwa wa kazi zote zinazohusiana na lugha, na
- kuelewa maneno au misemo inayotumiwa, ambayo baadhi yake inaweza kuwa ya kipekee kwa Kanada tu.

Kama unaweza, jaribu kutambua mahitaji ya lugha yanayohitajika kufanya kazi katika fani yako. Mara ufikapo Kanada, mdhamini wako anaweza kukusaidia kujiandikisha kwenye madarasa ya lugha. Wadhamini wako wanaweza pia kukuunganisha na watoa huduma ambao wanatoa mafunzo ya bure ya taarifa au huduma binafsi ili kukusaidia kupata kazi.

Kama una shahada ya chuo kikuu, diploma ya chuo au cheti cha biashara, kinaweza kisikubalike Kanada. Itakuwa ni juu ya serikali ya mkoa au bodi ya udhibiti ya sehemu ambayo utakaa kuamua kama shahada / cheti au hati nyingine zinatambulika. Watoa huduma pia wanaweza kukusaidia kukuongoza katika mchakato huu.

Kujitolea pia ni njia nzuri ya kupata uzoefu wa kazi Kanada. Ingawa ukijitolea hulipwi, kutakusaidia kuboresha ujuzi wako wa lugha na unaweza kupata ujuzi muhimu wa kuomba kazi. Pia ni njia nzuri ya kupata marafiki na kukutana na watu katika jamii yako.

## Huduma za makazi

Huduma za makazi zinafadhiliwa na Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Kanada – IRCC (na Ministère de l'Immigration, de la Diversité et de l'Inclusion , Quebec) na zinapatikana  kwa wakazi wote wa Kanada wa kudumu, ikiwa ni pamoja na  wakimbizi waliopatiwa makazi. Huduma hizi ni bure na zinaweza kukusaidia kujiandaa vizuri na maisha nchini Kanada.

Kuna huduma nyingi kwenye mtandao za kujiandaa na safari ambazo zinapatikana kwenye tovuti ya Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Kanada  kukuandaa kuishi Kanada. Unaweza kupata huduma hizi mara tu utakapothibitishiwa kwamba  maombi yako yamekubalika.

Mara tu ufikapo Kanada, wataalamu wa makazi watakupatia huduma mbalimbali za bure ili uweze kuishi nchini Kanada. Hizi ni pamoja na msaada wa kutafuta kazi, mafunzo ya lugha, mafunzo maalumu ya kazi, huduma kwa vijana na wazee, na zaidi.

Orodha kamili ya huduma za makazi zinazodhaminiwa na Uhamiaji, Wakimbizi, na Uraia Kanada inaweza kupatikana mtandaoni.

## Matumizi

Utakapofika Kanada, utapatiwa msaada wa kifedha kutoka  serikali ya Kanada kwa miezi 6 na kutoka kwa wadhamini wako binafsi kwa muda wa miezi 6 iliyobaki , au mpaka utakapoweza kujitegemea - chochote kitakachoanza kwanza.

Mara msaada kutoka kwa mfadhili wako binafsi na serikali kuisha, utakuwa na jukumu la kulipia gharama zako mwenyewe, ikiwa ni pamoja na chakula, pango, umeme, maji, nguo na kodi. Ni muhimu kujifunza namna ya kuipangia matumizi hali yako.

Kama hutoweza kupata kazi baada ya miezi 12 na unahitaji msaada kusaidia familia yako, kuna aina mbalimbali za huduma za jamii, kama mabenki ya chakula na mashirika ya msaada kwa mahitaji hayo. Pia kuna programu za misaada mbalimbali ya kifedha inayotolewa na serikali kwa watu wanaohitaji, hata hivyo ni lazima uwe na vigezo fulani ili kufaidika na programu hizi.  Waulize wadhamini wako kwa taarifa zaidi kuhusu ni msaada gani unapatikana kwenye jamii yako.

Unaweza pia ukataka kutuma fedha  kwa familia yako nyumbani. Upo huru kufanya hivyo, lakini watu wengi wanashindwa kujikimu wenyewe na bado wana pesa ya kutuma nyumbani. Nchini Kanada, vitu vingi vinaweza kuhitaji fedha zaidi kuliko ulivyozowea kulipia. Kumbuka kwamba itachukua muda kuzoea maisha mapya ya Kanada.

## Shule



Hutolazimika  kulipia watoto wako kwenda shule ya msingi au sekondari. Watoto wote kati ya miaka 6 na 16 ni lazima waende shule. Ni sheria. Wanafunzi wengi huhudhuria shule ya sekondari mpaka wanapohitimu diploma (wakiwa na miaka 18).

Baada ya kumaliza shule ya sekondari, watoto wako wanaweza kwenda chuo kikuu au chuo. Chuo na chuo kikuu  ni gharama, lakini chuo au chuo kikuu wanaweza kuwa na rasilimali za kuwasaidia kupata udhamini, ruzuku au mkopo wa mwanafunzi.

## Afya na huduma za meno



AKama mkazi wa kudumu wa Kanada,  huhitajiki kulipia huduma nyingi za afya, ikiwa ni pamoja na  kwenda hospitali au kumuona daktari.

Unapofika Kanada, utapatiwa bima ya Programu ya Afya ya Mpito ya Serikali (IFHP). Bima ya IFHP inatoa huduma muhimu za afya (ikiwa ni pamoja na kumuona daktari au kwenda hospitali) mpaka utakapoweza kupata bima ya jimbo au wilaya husika, ambayo inapatikana hasa ndani ya ya miezi mitatu (3). Wakati huu, ni lazima uombe bima ya afya kwenye mkoa au wilaya unayoishi.

Ni muhimu kuwakilisha nyaraka zako za kustahiki IFHP kwa mtoa huduma wa afya kila wakati unapoenda kumuona. Unaweza kupata huduma za afya mahali popote Kanada kutoka kwa mtoa huduma yoyote wa afya ambaye amesajiliwa. Orodha ya watoa huduma waliosajiliwa inapatikana mtandaoni chini ya orodha ya "Tafuta watoa  huduma IFHP".

IFHP pia wanatoa bima za dawa na  bima za ziada, ili kushughulikia mahitaji mbalimbali ya dharura na huduma za afya za msingi (kwa mfano, huduma za afya ya akili, baadhi ya huduma za macho na huduma ya haraka ya meno  kwa ajili ya kupunguza maumivu na maambukizi).  Bima za dawa za ziada na za kuandikiwa  zinatolewa endapo tu kama unapokea msaada kutoka wadhamini wako binafsi.

Muhtasari wa faida na huduma zote za IFHP zinapatikana kwenye tovuti ya  Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Kanada (IRCC).

Wadhamini wako wanaweza kukusaidia kuchagua daktari wa familia, kutafuta daktari wa meno, na kukuunganisha kwenye ushauri wa afya ya akili na maumivu sugu  itakapohitajika.

Kila mkoa na wilaya wana programu yao ya bima. Hakikisha unafahamu bima yako inalipia nini. Wadhamini wako watakusaidia kuomba hati muhimu zinazohitajika utakapofika Kanada.

Wakimbizi ambao ni wapya Kanada mara nyingi wanajisikia upweke na kutengwa, na wanaweza kuwa na msongo wa mawazo kutokana na maumivu ya matukio ya zamani. Kuna huduma nyingi za bure na watu waliofundishwa kuzungumza wanaoweza kukusaidia kupona maumivu yako.  Kama unatafuta msaada, waulize wadhamini wako kuhusu huduma za afya na ushauri wa akili zinazopatikana kwa ajili yako.

## Chanjo

Kupata chanjo dhidi ya ugonjwa ni njia mojawapo na salama ya kuzuia magonjwa, matatizo ya afya na kifo cha mapema.

Chanjo inafanyakazi kwa kusaidia kujenga mfumo wa kinga wa mwili wako. Kama dawa zote nchini Kanada, chanjo zimepitia mchakato kamili wa kuzithibitisha na kuzipitisha kabla ya kutolewa kwa umma.

Jopo la madaktari wanaweza kukupa chanjo kusasisha hali yako ya chanjo wakati wa uchunguzi wa matibabu ya uhamiaji, kabla ya kufika Kanada. Huduma hizi ni za hiari. Ikiwa utachagua kupata chanjo nje ya nchi, unapaswa kuleta rekodi yako ya chanjo Kanada.

Mara ufikapo Kanada, chanjo nyingi zinalipiwa na programu yako ya mji au wilaya. Wewe na familia yako mnaweza kuwa na magonjwa ambayo chanjo inaweza kuyazuia, hasa kama hukuwahi kupatiwa chanjo siku za nyuma. Watoto wachanga na watoto wadogo huweza kuambukizwa magonjwa kadhaa, na baadhi ya maeneo ya Kanada, watoto wanahitaji kupatiwa chanjo zao kwa wakati uliopangwa kabla ya kuanza shule au huduma ya kuangaliwa kwa siku.

Mdhamini wako, daktari au kliniki ya afya wote wanaweza kutoa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kusasisha hali yako ya chanjo.

Ni uamuzi binafsi wa kuamua mwenyewe na / au familia yako kupata chanjo. Lakini kumbuka: unapopata chanjo, unajilinda wewe na wengine dhidi ya magonjwa maalumu na kusaidia kuzuia kuenea kwa magonjwa kwa wale ambao wapo hatarini zaidi.

## Chakula na maji



Maji nchini Kanada ni salama kwa kunywa. Kila nyumba ina maji yake ya moto na ya baridi. Unaweza kupata maji wakati wowote mchana au usiku.

Aina mbalimbali za chakula zinapatikana kununua itategemea na jamii yako. Miji mikubwa na tofauti ya Kanada itakuwa na vyakula vingi ambavyo unakula kwa kawaida, wakati jamii ndogo zinaweza kuwa na machaguo machache.

Watu kutoka makabila mengi wanaishi Kanada, hivyo inamaanisha kuna vyakula vingi mbalimbali kutoka tamaduni nyingi, na unaweza kupata maduka maalumu kwa bidhaa maalumu za chakula. Baadhi ya vyakula vingine vinaweza kuwa ghali zaidi kuliko ulivyozowea kutokana na hali ya hewa ya Kanada na mahitaji ya kuagiza baadhi ya vyakula.

## Dini






Dini nyingi zipo Kanada. Upo huru kuabudu dini yako. Sheria ya Kanada inahitaji kuheshimu watu wanaoabudu dini tofauti. Hutoombwa wala kulazimishwa kubadilisha dini yako. Uhuru wa dini ni mojawapo ya haki za msingi Kanada.

Japokuwa wadhamini wengi binafsi wanahusishwa na vikundi vya imani, unaweza kuendelea kuabudu dini yako. Watu hawa wamejitolea ambao wanataka kukusaidia kuja Kanada na kujumuika vizuri, bila ya kipingamizi.

## Hali ya hewa









Kuna misimu minne (4) tofauti nchini Kanada: vuli, majira ya joto, kipupwe na majira ya baridi. Kanada ni nchi kubwa sana na hali ya hewa kila msimu inaweza kuwa tofauti kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine.

Vuli (Machi, Aprili na Mei) ni msimu wa mvua katika sehemu nyingi za Kanada, na hali ya hewa inaweza kuwa ya baridi. Katika majira ya joto (Juni, Julai na Agosti), hali ya hewa ni joto sana katika maeneo mengi ya nchi. Wakati wa mchana, joto mara nyingi ni zaidi ya 20°C na mara nyingi huongezeka juu ya 30°C.

Wakati wa kipupwe (Septemba, Oktoba na Novemba), hali ya hewa ni ya baridi na pia kunaweza kuwa na mvua nyingi. Katika miezi ya baridi (Disemba, Januari na Februari) ni baridi sana katika maeneo mengi, na joto mara nyingi ni chini ya 0°C. Theluji hufunika ardhi kuanzia Disemba hadi Machi au Aprili. Kusini magharibi mwa British Columbia (karibu na Victoria na Vancouver), katika kipindi cha majira ya baridi ni kawaida kuwa na mvua kuliko theluji.

Kulingana na wapi unatoka, kwa mara yako ya kwanza unaweza kushangazwa sana na baridi na theluji wakati wa baridi Kanada. Ukiwa na mavazi yanayostahiki, utakuwa tayari kufurahia uzuri wa kipekee wa baridi ya Kanada. Mdhamini wako atakusaidia kupata kofia, buti, glovu na nguo za baridi kwa familia yako.

## Maneno ya mwisho ya ushauri

Kuanza maisha mapya nchini Kanada kunasisimua na kuna fursa nyingi mpya. Hata hivyo kutakuwa na changamoto pia. Baadhi ya watu huwa ni vigumu kuzowea. huchukua muda, hivyo jaribu kuwa mvumilivu. Kumbuka kwamba wageni wengi kama wewe wamezowea na wamejumuika kikamilifu na jamii ya Kanada.

Kuna watu na huduma zinazopatikana ili kukusaidia. Mdhamini wako anapatikana kujibu jambo lolote au maswali utakayokuwa nayo. Wanaangalia sana maslahi yako zaidi. Unaweza pia kuwasiliana na ofisi za Uhamiaji, wakimbizi na Uraia Kanada (IRCC) kwa maswali kuhusu maombi yako.

Rasilimali nyengine ni pamoja na vikundi vya jamii, makundi ya dini huduma za ushauri na makazi yanayodhaminiwa na mashirika ya serikali. Makundi haya yote yana uzoefu wa kuwasaidia wageni kuzoea kwa njia tofauti. Usiogope kuomba msaada.

Ukifikia hatua unaamini umetendewa sivyo au kudhulumiwa, au hupati msaada wa kutosha ulioahidiwa na wadhamini wako, tafadhali wasiliana na Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Kanada haraka iwezekanavyo kwenye IRCC.INPSR-PPPRRI.IRCC@cic.gc.ca.

Hautoweza kupoteza msaada wako wa kifedha au halii yako ya Uhamiaji, Ukimbizi na Uraia Kanada.

Mwisho, kuna tovuti zenye taarifa nyingi zaidi za kukusaidia kujiandaa. Tovuti za mkoa zina taarifa nyingi za muhimu, ikiwa ni pamoja na maswali yaulizwayo mara kwa mara, viunganisho vya jamii, habari na matukio.

Tovuti ya Serikali ya Kanada ina maelezo zaidi juu ya maisha ya Kanada, orodha na ramani ya mashirika ya huduma za makazi katika jamii zote nchini, taarifa kuhusu tathmini za bure za lugha, na rasilimali za ziada kujiandaa kwa ajili ya safari yako kuja Kanada.

**www.canada.ca/immigration**